

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

610

UALIMU

Muda: Saa 3

Jumanne, 08 Mei 2012 asubuhi

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na swali **moja (1)** kutoka kila sehemu B, C, D na E.
3. Sehemu A ina alama 40, sehemu B, C, D na E zina alama 15 kila moja.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Orodhesha mbinu nne zinazoweza kutumika kupata taarifa mbalimbali za mwanafunzi.
2. Bainisha mbinu nne ambazo Mwalimu Mkuu anaweza kuzitumia ili shule iwe na mazingira ya kuvutia katika ufundishaji na ujifunzaji.
3. Kiwango cha ugumu wa swali la kwanza na la pili katika mtihani wa somo la Muziki kilikuwa kama ifuatavyo:

Swali	Kiwango cha Ugumu %
1.	86
2.	52

(a) Tafsiri matokeo hayo.

(b) Orodhesha faida mbili za kuchanganua swali.

4. Bainisha vitendo vinne afanyavyo mtoto mchanga ambavyo havitokani na kujifunza na wala havitawaliwi na utashi wake.
5. Chora jedwali lifuatalo kisha andika tofauti mbili kati ya kitabu cha mwalimu na kiongozi cha mwalimu.

Na.	Kitabu cha Mwalimu	Kiongozi cha Mwalimu
1.		
2.		

6. Taja mikakati minne iliyotumika kuimarisha elimu ya watu wazima nchini Tanzania katika miaka ya 1970.
7. Andika sababu mbili za kutumia tathmini tamati katika kutathmini mtaala.
8. Kwa kutumia mfano, eleza dhana ya "mkoba wa kazi" kama inavyotumika katika upimaji na tathmini.
9. Orodhesha adhabu nne zinazoweza kutolewa na Tume ya Walimu Tanzania kwa mwalimu anayekiuka maadili ya kazi ya ualimu.
10. (a) Ni mbinu gani ya unasihi inaweza kutumika ili kumsaidia mwanafunzi mwenye tatizo lakini yeye mwenyewe hahisi kama analo tatizo.
(b) Toa sababu mbili za kuchagua mbinu ya unasihi uliyoitaja katika kipengele 10 (a).

SEHEMU B (Alama 15)

SAIKOLOJIA YA ELIMU

Jibu swali moja (1) kutoka katika sehemu hii.

11. Bainisha hatua za ukuaji wa mtoto kulingana na mwanasaikolojia Jean Piaget. Eleza wazi umuhimu wa kielimu kwa kila hatua husika.
12. Kwa kutumia mifano, fafaua sababu tano zinazoweza kuathiri uwezo wa mtoto katika kujifunza.

SEHEMU C (Alama 15)

MITAALA NA UFUNDISHAJI

Jibu swali moja (1) kutoka katika sehemu hii.

13. Eleza mapungufu manne yanayoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya njia ya igizo dhima katika kufundisha na kujifunza.
14. Kwa kutumia mifano, oneshwa jinsi tathmini endelevu inavyotoa mrejesho kwa mwalimu na mwanafunzi. Andika hoja tatu kwa upande wa mwalimu na tatu kwa mwanafunzi.

SEHEMU D (Alama 15)

UTAFITI WA KIELIMU, UPIMAJI NA TATHMINI

Jibu swali moja (1) kutoka katika sehemu hii.

15. Alama zifuatazo ni za wanafunzi wa Shule ya Msingi Upendo walizopata katika somo la Stadi za Kazi.

82	82	72	72	72	72	77	67	67	67
57	57	57	57	57	62	62	62	62	62
62	52	52	52	52	52	42	42	42	42
42	47	47	47	37	37	37	32	32	27

Kutokana na mtawanyiko wa alama ghafi za hao wanafunzi, tafuta:

- (a) Wastani
- (b) Marudio ya kila alama.
- (c) Variansi
- (d) Achano sanifu.

16. Wanafunzi wa shule ya msingi ya Mshikamano wamepewa maelekezo na vifaa vya kufanya kazi kwa vitendo. Bainisha mambo muhimu manne ya kuzingatia katika kuwapima uwezo wao katika kazi ya vitendo.

SEHEMU E (Alama 15)

MISINGI YA ELIMU

Jibu swali **moja (1)** kutoka katika sehemu hii.

- ✓17. Eleza kwa ufasaha sababu tano zinazofanya ualimu uwe kazi ya kitaalamu.
18. Eleza kwa kutumia hoja tano jinsi ambavyo elimu ingeweza kutumika katika kuendeleza sera ya Ujamaa na Kujitegemea kwa Watanzania kama ilivyotamkwa katika Azimio la Arusha 1967.